JAMHURI YA KENYA
WIZARA YA ELIMU

# MTAALA WA SHULE YA MSINGI

# KISWAHILI

## GREDI YA 3

## KWA WANAFUNZI WALIO NA CHANGAMOTO ZA KUONA

**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**
***JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI***

Chapisho la Kwanza  2017

Chapisho la Pili 2022

Chapisho la Tatu 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-43-069-1**

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

**DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU**

Serikali ya Kenya inajitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo, na utafiti yanakidhi matarajio ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala wa Kitaifa ya 2019, Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Kenya imesaini. Kuelekea kufikia lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu (MoE) imetekeleza kwa mafanikio na hatua kwa hatua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi (CBC) katika ngazi ya awali, msingi, na Shule za Upili za daraja la chini.

Utekelezaji wa Mtaala wa Kitaalamu unajumuisha ufuatiliaji na tathmini ili kubaini mafanikio yake. Baada ya mzunguko wa miaka mitano wa utekelezaji, tathmini ya jumla ya mzunguko wa elimu ya msingi ilifanywa ili kubaini kufikia malengo ya matokeo ya kujifunza kama ilivyotarajiwa katika Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Msingi.

Serikali ya Kenya iliunda Jopo Kazi la Rais kuhusu Mageuzi ya Elimu'Presidential working party on Education Reforms' (PWPER) mwaka 2022 kushughulikia masuala muhimu yanayoathiri sekta ya elimu. PWPER ilifanya mapendekezo mbalimbali yaliyochangia marekebisho ya mtaala.

Mapendekezo ya PWPER, ripoti za ufuatiliaji, tathmini ya jumla, maoni kutoka kwa watekelezaji wa mtaala, na wadau wengine yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa.

Mtaala wa Gredi ya **3** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona uliofanyiwa marekebisho, umejengwa kutokana na umilisi uliokuzwa katika gredi ya **Pili**. Umuhimu katika gredi hii ni maendeleo ya usomaji wa msingi, hesabu, na stadi za mwingiliano na mazingira.

Mitaala hii inawakilisha Malengo ya Kitaifa ya Elimu, kauli kiini, matokeo yanayotarajiwa kwa ujumla na kwa kila somo pamoja na Mada na Mada Ndogo. Mitaala hiyo pia inajuimuisha Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa , Swali Dadisi Lililopendekezwa, Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:, masuala mtambuko (PCI's), maadili, vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Nina matumaini kwamba mashirika yote ya serikali na wadau wengine katika Elimu watatumia miundo hii kubuni ufanisi na ufanisi utekelezaji wa CBC.

**MHE. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU,**
**WIZARA YA ELIMU**

**DIBAJI YA KATIBU MKUU**

Wizara ya Elimu (MoE) ilianza kutekeleza Mtaala wa Kiumilisi (CBC) mwaka 2019 nchini kote. Gredi ya **Kwanza** ndiyo ya kwanza katika ngazi ya Elimu ya daraja ya awali nayo Gredi ya **Sita** ni ya mwisho katika ngazi hiyo katika mfumo uliofanyiwa marekebisho wa elimu.

Mtaala uliofanyiwa marekebisho wa Gredi **ya 3** unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Umilisi kutoka Gredi ya 2 **katika** ngazi ya Msingi. Mtaala huu unatoa fursa kwa wanafunzi kuzingatia wanachokipenda ili kuunda msingi wa elimu na mafunzo zaidi na/au kupata stadi za ajira. Kiwango hiki cha elimu ni muhimu sana katika kuchangia kufikia ruwaza na mwito wa marekebisho yanayoendelea ya kimtaala kama ilivyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Kuelekea kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora, faafu na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya ''*Towards Realizing Quality, Relevant and Inclusive Education and Training for Sustainable Development'*. Mswada Elekezi huo unaeleza kuhusu kuvuka kutoka mtaala wa Kimafunzo na kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi.
Hivyo basi, mtaala wa Gredi ya **3** kwa wanafunzi walio na *changamoto za kuona* inalenga kuimarisha ukuzaji wa Umilisi wa Kimsingi katika mtaala huu, yaani: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya kuendelea kujifunza na kujiamini.
Mitaala inapendekeza shughuli shirikishi za ujifunzaji unaolingana na Mada Ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya mtaala wa umilisi (CBC). Pia inapendeza baadhi ya nyenzo za kufundishia na mbinu za kutathmini mbalimbali. Inatarajiwa kwamba mitaala hii itaongoza walimu kufanikisha wanafunzi kufikia Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa ya kujifunza katika gredi ya **3** na kuwaandaa kwa mpito laini kwa Gredi ya **4**. Zaidi ya hayo, ni matumaini yangu kuwa mwalimu atatumia mitaala iliyobadilishwa kufanya ujifunzaji uwe wa kuvutia unaochangamsha na wa kufurahiwa.

**DKT. BELIO KIPSANG', CBS**

**KATIBU MKUU**

**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

**SHUKRANI**
Sheria Nambari 4 ya 2013 (Toleo jipya 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) inaipa uwezo Taasisi kukuza na kuipitia Mitaala*(SNE adapt)* na vifaa vya msaada kwa mtaala wa elimu ya msingi na ya vyuo vya Elimu na Mafunzo ya juu vilivyo chini ya vyuo vikuu. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote huhusisha utafiti, ulinganishi wa kimataifa, na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato huu wa utaratibu na wa mashauriano, KICD ilizua wazo la Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) 2017 ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.(SGDs)
.
Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) hufadhiliwa na Serikali ya Kenya ili kutekeleza majukumu na mipangilio ya serikali na sekta ya elimu. Pia, Taasisi hupata msaada kutoka kwa mashirika mengine ya kimaendeleo yanayoangazia miradi teule.
Mtaala uliyorekebishwa gredi ya **tatu** kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona ilipangwa na kubadilishwa kwa msaada wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Usawa wa Elimu ya Msingi ya Kenya katika Programu ya Kujifunza ‘Kenya Primary Education Equity in Learning Programme’ (KPEELP); mradi ulioratibiwa na MoE. Kwa hiyo, Taasisi inashukuru sana kwa msaada wa Serikali ya Kenya, kupitia MoE, na washirika wa maendeleo kwa msaada wa sera, rasilimali, na msaada wa logistiki. Kwa namna ya pekee, shukrani maalum kwa Waziri wa Elimu-MoE na Katibu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi.

Pia ningependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wanaelimu wengine walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia mashirika mengine yanayoshirikiana na serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa majukumu mbalimbali waliyotekeleza katika ukuzaji na ubalishaji wa Mitaala ya Gredi ya 4-6 kwa wanafunzi walio na changamoto za kuona. Kuhusiana na hili, ningependa kushukuru Katibu wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC) kwa msaada wao katika mchakato wa kukuza na kubadilisha mitaala hii. Mwisho, ninawashukuru sana mwenyekiti wa baraza la KICD na wanachama wengine wa Baraza kwa mwongozo thabiti katika mchakato huu.
Nawahakikishia watekelezaji wa mtaala, wazazi na washikadau wengine kuwa mitaala hii itaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya tatu na maandalizi ya wanafunzi walio na changamoto za kuona kwa mpito wa sekendari ngazi ya chini.

**PROF. CHARLES O. ONG’ONDO, PhD, MBS**

**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU**
**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

**YALIYOMO**

UTANGULIZI ........ **Error! Bookmark not defined.**
DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU ........ iii
DIBAJI YA KATIBU MKUU ........ iv
YALIYOMO ........ v
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ........ vi
MGAO WA VIPINDI ........ vii
MATOKEO MAALUM YA UJIFUNZAJI YANAYOTARAJIWA KATIKA ELIMU YA MSINGI ........ viii
MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI ........ viii
1.0 UZALENDO ........ 1
2.0 SHAMBANI ........ 10
3.0 MIEZI YA MWAKA ........ 23
4.0 KAZI MBALIMBALI ........ 34
5.0 USALAMA ........ 45
6.0 USAFI WA MAZINGIRA ........ 54
7.0 DUKANI ........ 66
8.0 NDEGE NIMPENDAYE ........ 74
9.0 SOKONI ........ 85
10.0 TEKNOLOJIA ........ 95
MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ........ 106
KIAMBATISHO I: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL) ........ 111
KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI ........ 113

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
   a) **Mahitaji ya kijamii**
      Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
      Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
      Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.
      Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko yanayoendelea ulimwenguni.
3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye

nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

**MGAO WA VIPINDI**

| **S/No** | **SOMO** | **Vipindi kwa wiki** |
|---|---|---|
| 1. | Braille literacy Activities | 2 |
| 2. | Kiswahili Language Activities for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 3. | English Language Activities for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 4. | Mathematical Activities for Learners with Visual Impairment | 5 |
| 5. | Religious Education Activities | 3 |
| 6. | Environmental Activities for Learners with Visual Impairment | 4 |
| 7. | Creative Activities for Learners with Visual Impairment | 7 |
| 8. | Pastoral/Religious Instruction Programme | 1 |
| **Total** | | **31** |

**MATOKEO MAALUM YA UJIFUNZAJI YANAYOTARAJIWA KATIKA ELIMU YA MSINGI**

Kufikia mwisho wa elimu ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kuwasiliana apasavyo akitumia mbinu za mazungumzo na ishara katika miktadha mbalimbali,
b) kutumikiza maarifa, ujuzi, maadili na mitazamo katika maisha ya kila siku,
c) kudhhihirisha ujuzi wa kijamii maadili, na maadili ya kidini kwa nia ya kuchangia kukua kwa jamii,
d) kukuza talanta kwa nia ya kujiendeleza na kujifanikisha,
e) kuafiti, kutumia, kulinda na kutunza mazingira kwa nia ya kujifunza na kwa maendeleo endelevu,
f) kutumia ujuzi wa kidijitali wenye teknolojia saidizi kujifunza na kujifurahisha,
g) kuthamini tamaduni mbalimbali kwa nia ya kuishi kwa amani,
h) kufurahia haja ya umuhimu wa kutegemeana kwa binadamu na mataifa.

**KAULI KIINI**

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi walio na changamoto za kuona wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika kiwango cha kwanza cha elimu. Somo hili humwezesha mwanafunzi aliye na changamoto za kuona kujenga stadi za kimsingi za Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma na Kuandika. Aidha, somo hili humwandaa mwanafunzi aliye na changamoto za kuona kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

**MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI**

Kufikia mwisho wa kiwango cha chini, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano,
b) kuzingatia kanuni za lugha ili kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi,
c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali,
d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani,
e) kutumia hati/nukta nundu zifaazo za kimaandishi na mfumo wa kidijitali wenye teknolojia saidizi kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali,
f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

**MADA**

Kusikiliza na Kuzungumza
Kusoma
Kuandika
Sarufi

| Mada | Mada Ndogo | Muda Uliopendekezwa |
|---|---|---|
| Kusikiliza na Kuzungumza | Maamkuzi na Maagano | 3 |
| | Matamshi Bora;vokali,konsonanti,/py/,/vy/,/sh/,/mbw/,/nd/,/ny/,/mb/,/nz/,/tw/ | 15 |
| | Maneno ya Heshima na Adabu | 3 |
| | Ufahamu wa Kusikiliza | 3 |
| | Maagizo | 3 |
| | Mazungumzo | 3 |
| Kusoma | Kusoma Ufahamu | 15 |
| | Kusoma kwa Ufasaha | 15 |
| Kuandika | Hati Nadhifu: Kifungu, Herufi kubwa, Herufi ndogo | 9 |
| | Nafasi ya Pambizo katika uandishi | 3 |
| | Matumizi ya Kiulizi | 3 |
| | Imla | 3 |
| | Uandishi wa Insha | 3 |
| | Tahajia | 3 |
| | Insha ya Masimulizi | 3 |
| | Insha ya Maelezo | 3 |
| Sarufi | Matumizi ya yeye na wao, yule na wale, hili na haya | 9 |
| | Umoja na Wingi wa Sentensi | 6 |
| | Matumizi ya -ake na -ao | 3 |
| | Matumizi ya -eupe, - eusi, - ekundu | 3 |
| | Ukanushaji wa nafsi ya tatu | 3 |
| | Matumizi ya juu ya, ndani ya, na mbele ya. | 3 |
| | Vinyume vya Vitendo | 3 |
| **Jumla ya Vipindi** | | **120** |

**Matokeo ya Kijumla Yanayotarajiwa Katika Kiwango cha Kwanza cha Masomo**

Kufikia mwisho wa kiwango cha kwanza cha masomo, mwanafunzi aweze:

a) kutumia mbinu zifaazo za usikivu katika mawasiliano kwenye mazingira yake,
b) kudhihirisha ufasaha wa kuzungumza kwa Kiswahili,
c) kusoma kwa ufasaha na kufahamu aina zozote za maandishi ya Kiswahili,
d) kuelezea mawazo, hisia na tajiriba kwa maandishi ya mkono au mbinu nyingine yoyote ya uwasilishaji,
e) kutumia sarufi ipasavyo katika mawasiliano,
f) kutumia msamiati ufaao katika mazingira yake kuwasiliana,
g) kuonyesha ukakamavu katika kuwasilisha masuala yanayomkabili na yanayokabili mazingira yake.

| **1.0 UZALENDO** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>c) kuthamini matumizi ya maamkuzi na maagano katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi aliye na upunguufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi na maagano (*k.v. Umeamkaje? Umeshindaje? Safiri salama, Mchana mwema, Usiku mwema)*, vitabu, kadi maneno, mti maneno, picha au michoro, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi na maagano *(k.v. Umeamkaje? Umeshindaje? Safiri salama, Mchana mwema, Usiku mwema)* kutoka kwenye chati, kadi maneno, mti maneno zilizo na maandishi ya breli, maelezo ya picha/ maelezo ya michoro, au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kujadili na wenzake picha, michoro, video n.k. zinazoonyesha vitendo vya maamkuzi na maagano. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kujadili na wenzake maelezo ya picha, michoro au video n.k. yanayoonyesha vitendo vya maamkuzi na maagano. | Ni vipi unaweza kuwaamkua au kuwaaga wenzako? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kuigiza maamkuzi na maagano akiwa na wenzake ili kujenga umilisi wa kutumia maneno haya. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe moja kwa moja kuigiza ishara za vitendo, mfano kupunga mkono kuashiria kwaheri.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii yake.<br>• Mwanafunzi amwamkue na kumuaga mzazi au mlezi kwa kutumia maamkuzi na maagano ya jamii yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuwasiliana na wenzake katika kujadili maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii zao.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza au kutazama maamkuzi na maagano.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika majadiliano.
- Hamu ya Ujifunzaji: mwanafunzi anaposikiliza kwa makini maamkuzi na maagano ya jamii yake.

**Maadili**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika mijadala ya maamkuzi na maagano darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia.
- Upendo: mwanafunzi anapozingatia maamkuzi na maagano katika jamii.
- Heshima: mwanafunzi anpotumia maneno ya heshima na adabu katika maamkuzi na maagano.

**Masuala Mtambuko**.

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi  anapomwamkua mzazi au mlezi wake kwa lugha ya kijamii.

| **Uhusiano na Masomo Mengine** |
|---|
| Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maamkuzi na maagano aliyojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji** |
| Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, chati/ chati za breli, mti maneno, picha / maelezo ya picha. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno 51- 54 kilichoandikwa kwa breli au fonti ifaayo na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v uzalendo, umoja, undugu, ushirikiano, upendo, n.k)* akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia msamiati wa suala lengwa katika mawasiliano.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu chenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au chati yenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kusikiliza maelezo ya picha kwenye kitabu chenye maandishi ya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au chati | 1. Je, kwa nini tunasoma hadithi?<br>2. Je, ni mambo gani unaweza kujifunza kutokana na hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yenye maandishi ya breli akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi na kifungu kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi kutambua msamiati kuhusu suala lengwa
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali vyenye teknolojia saidizi kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma kifungu ili kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu: mwanafunzi anapo tunga sentensi na kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotoa hoja zake kwa wenzake na anaposhirikisha mzazi au mlezi wake kusoma na kujadili kifungu.

**Maadili**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi kujadiliana.
- Heshima: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kusoma kifungu darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali.

**Masuala Mtambuko**

- Usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika shughuli za ujifunzaji
- Masuala ya Afya: mwanafunzi anapojifunza kuhusu mimea na matunda mbalimbali yanayopatikana shambani.
- Haki za kijamii: mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika shughuli za kikundi wakiwepo walio na changamoto za kimaumbile.

| |
|---|
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu (aliye na upungufu wa kuona)<br>b) kutambua mambo yanayozingatiwa kufanikisha maandishi ya breli nadhifu,(asiyeona),<br>c) kuandika kifungu cha maneno kati ya | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua mambo mbalimbali yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu *(k.v. muundo wa herufi, nafasi ifaayo kati ya maneno, nafasi zifaazo pambizoni, kutenganisha sentensi ifaavyo, usafi wa nakala n.k.)* kutoka kwenye kitabu, chati, zilizoandikwa kwa fonti ifaayo, au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake.<br>Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua mambo mbalimbali yanayozingatiwa kufanikisha maandishi ya breli nadhifu (*k.v. mpangilio mwafaka wa nukta nundu kuunda herufi, nafasi ifaayo kati ya maneno, nafasi zifaazo pambizoni, kutenganisha sentensi ifaavyo, usafi wa nakala n.k.*) kutoka kwenye kitabu cha breli, chati, yenye maandishi ya breli, kadi za breli au vifaa vya | Ni vipi tunavyo fanikisha maandishi nadhifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 25-30 kwa hati nadhifu,<br>d) kuandika kifungu cha maneno kati ya 25-30 kwa maandishi ya breli nadhifu,<br>e) Kufurahia kuandika kwa hati au maandishi ya breli nadhifu ili kunufaisha mawasiliano. | kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kunakili kifungu cha maneno yasiyozidi 30 kwa hati nadhifu kutoka kwenye kitabu, chati zilizo na fonti zifaazo au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi *n.k.* Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kunakili kifungu cha maneno yasiyozidi 30 kwa maandishi ya breli nadhifu kutoka kwenye kitabu, chati zilizo na maandishi ya breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknoloji saidizi n.k.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 30 akizingatia hatua za uandishi nadhiifu *(k.v. maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake, mzazi au mlezi kutambua hati nadhifu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyeneye teknolojia saidizi katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli mbalimbali za kuandika.
- Ubunifu: mwanfunzi anapoandika kifungu kwa hati nadhifu.

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutumia vifaa vya kidijitali kutambua mambo mbalimbali ya kuzingatiwa kufanikisha maandishi.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kwa utulivu.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli ya kuandika.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika mambo mbalimbali kuhusu suala lengwa.<br>● Uwekaji wa akiba: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu jinsi ya kutunza rasilimali. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kuandika kwa hati nadhifu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/ chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/kadi za maneno za breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | 1.4.1 Matumizi ya **yeye** na **wao**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua neno yeye na wao katika sentensi,<br>b) kutumia neno yeye na wao ipasavyo katika sentensi,<br>c) kufurahia kutumia neno yeye na wao katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu au wimbo unaohusu nafsi ya tatu (**yeye** na **wao**) kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutambua neno **yeye** na **wao** kutoka kifungu alichokisikiliza.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma vifungu vilivyo na nafsi ya tatu akiwa na wenzake au katika kikundi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujaza mapengo kwa kutumia yeye na **wao.**<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutumia nafsi ya tatu umoja na wingi kwa kuigiza mazungumzo na wenzake katika kikundi k.v. *Yeye anasoma - wao wanasoma.* Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia ishara katika kuiga mazungumzo mfano, kushiria kwa kidole kuonyesha nafsi ya tatu. | Ni vipi utaweza kutumia maneno yeye na wao katika sentensi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutoa mifano kwa kutumia yeye na wao.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya yeye na wao.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza matumizi ya yeye na wao.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia yeye na wao ifaavyo. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapouheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Uwajibikaji:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi kwa kutumia maneno yanayotaja nafsi ya tatu umoja na wingi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi huku akisikiliza michango yao na kutoa maoni.<br>● Amani: mwanafunzi anapozungumza na wenzake kuhusu suala lengwa. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapojenga mazoea ya kusoma na kuwa kielelezo katika jamii. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya maneno yeye na wao aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/ kadi za maneno ya breli, mti maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| 2.0 SHAMBANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Matamshi Bora:** Vokali na Konsonanti za Kiswahili<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua vokali za Kiswahili katika matini,<br>b) kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili katika matini,<br>c) kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>d) kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>e) kuchangamkia kutamka sauti za Kiswahili ili kuboresha matamshi. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vokali za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutatamka ipasavyo vokali za Kiswahili.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili (a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n,ng, ng’, ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z) zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi na kutambua vokali na konsonanti.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua | Vokali na konsonanti za kiswahili hutumika vipi katika matamshi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vokali na konsonanti za Kiswahili katika kifungu kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi peke yake, akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka maneno, sentensi au kifungu chenye sauti za Kiswahili akiwa peke yake au na wenzake katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujirekodi akitamka sauti za Kiswahili akitumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi na kujitathimini pamoja na kutathminiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka sauti za kiswahili ipasavyo naye mzazi au mlezi ampe maoni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuzisikiliza, kuzitambua na kuzitamka vokali na konsonanti za Kiswahili.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili na kujirekodi akizitamka.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapozitamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwa mzazi au mlezi wake ipasavyo. |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wanzake katika shughuli za kutamka vokali na konsonanti za kiswahili kwenye kikundi kwa utulivu.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakiwemo walio na changamoto za kimaumbile.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kutamka sauti za Kiswahili. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii na taifa; mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo mbalimbali kutambua na kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kutamka ipasavyo vokali na konsonanti za Kiswahili aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa, chati/ chati za breli |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2 Kusoma kwa Ufasaha:** *Sauti /**bw/, /fy**/ na /**kw/*** <br><br> (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sauti lengwa ***(/bw/, /fy/, /kw/)*** katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu chepesi chenye fonti ifaayo na isiyotatiza cha maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha breli cha maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kutoka katika kitabu chenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 47 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi) akiwa peke yake, au na wenzake. | Ili kufanikisha mawasiliano unastahili kusoma vipi ? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kutoka kwenye kitabu cha breli kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 47 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi) akiwa peke yake, au na wenzake.<br>• Mwanafunzi mwenye upungufu wa kuona asome hadithi kutoka kwenye kitabu chenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza, kifaa cha kidijtali chenye teknolojia saidizi, n.k. akiwa peke yake, au na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo.Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu cha breli, kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi, n.k. akiwa peke yake, au na wenzake akizingatia sauti inayosikika matamshi bora, kasi ifaayo na ishara/toni zifaazo.<br>• Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma kwa ufasaha akiwa na wenzake ,.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali vyenye teknolojia saidizi kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti /**bw/, /fy/** na /**kw**/ akizingatia matamshi bora, sauti inayosika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anaposoma akitumia ishara na sauti inayosikika kulingana na hadhira au masafa baina yake na anayemsikiliza. |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua sauti lengwa kwa ufasaha.<br>● Heshima: mwanafunzi anawaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia kujifunzia.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutumia vifaa vya kidijitali darasani. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma hadithi yenye sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali azingatie hatua za kiusalama.<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposoma kifungu na wenzake kutoka jamii mbalimbali kuhusu swala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya |

| |
|---|
| kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndongo | Matokeo Malum Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati Nadhifu:** Herufi Kubwa (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua herufi kubwa kwenye kifungu,<br>b) kutambua nukta nundu za herufi kubwa kwenye kifungu,<br>c) kuandika kifungu cha hadithi akitumia herufi kubwa,<br>d) kuandika kifungu cha hadithi akitumia nukta nundu za herufi kubwa,<br>e) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi kubwa katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusikiliza na kufuata kwa vidole uendelezaji ufaao wa mpangilio wa nukta nundu za kuandika herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua herufi kubwa katika kifungu kilichoko kwenye kitabu, chati, zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi n.k. akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nukta nundu za herufi kubwa katika kifungu kilichopo kwenye kitabu, chati zilizo na maandishi ya breli au kifaa cha | Je,herufi kubwa hutumiwa vipi katika maandishi ? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kidijitali chenye teknolojia saidizi n.k. akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa nukta nundu za herufi kubwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu chenye maneno **25-30** akizingatia maumbo ya herufi kubwa ifaavyo akizingatia hatua za uandishi (maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake).<br>● Mwanafunzi awaonyeshe wenzake, mzazi au mlezi wake kifungu alichokiandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kuandika herufi kubwa ,.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi wake kifungu alichokiandika akitumia maumbo ya herufi kubwa.<br>● Kujiamini:mwanafunzi anapofaulu kuandika maumbo ya herufi kubwa ipasavyo. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika kifungu wakizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa wa herufi kubwa.<br>● Umoja:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kutathmini herufi kubwa alizoziandika. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kuandika kifungu kifupi kwa mpangilio ufaao wa herufi kubwa kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kuandika kwa kutumia hati nadhifu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi** *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kutunga sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye kitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, akiwa peke yake, au na wenzake *(k.m. mimi ninapanda mti- sisi tunapanda miti, mimi ninapenda kulima - sisi tunapenda kulima).* Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye kitabu , chati zilizo na maandishi ya breli au maelezo ya chati, kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au katika vikundi *(k.m. mimi ninapanda mti- sisi tunapanda miti, mimi ninapenda kulima - sisi tunapenda kulima).*<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi katika umoja na wingi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi | Je, kwa nini unahitaji kutaja vitu katika hali ya umoja na wingi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | katika umoja na wingi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuambatanisha umoja na wingi wa sentensi alizopewa kwenye kitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuambatanisha umoja na wingi wa sentensi alizopewa kwenye kitabu, chati zilizo na maandishi ya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza michezo inayohusisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe jinsi ya kutumia ishara mbalimbali ili kuigiza sehemu yake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi katika umoja na wingi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi awasiliane na mzazi au mlezi wake akitumia sentensi katika hali ya umoja na wingi ipasavyo. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , na kuchangia kikamilifu katika kuandika sentensi katika umoja na wingi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoeleza kuhusu vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi katika umoja na wingi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapowasiliana na mzazi au mlezi akitumia sentensi katika hali ya umoja na wingi katika mazungumzo ya kila siku. |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , kusoma sentensi katika hali ya umoja na wingi.<br>● Uwajibikaji; mwanafunzi anapotunza nyenzo zinazotumiwa katika ujifunzaji wa sentensi za umoja na wingi.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi; mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi akizingatia mada lengwa kutoka kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuelewa maana ya kutunza mazingira. k.m. m*imi ninapanda mti – sisi tunapanda miti*.<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine , wanapotambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye nyenzo. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya umoja na wingi wa sentensi aliojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| 3.0 MIEZI YA MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Heshima na Adabu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu katika matini,<br>b) kutumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutazama michoro, picha au video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona apewe maelezo ya michoro, picha au asikilize video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua maneno ya adabu na heshima (tasfida) *k.v. kwenda msalani, haja kubwa, haja ndogo, kuendesha* kutoka kwenye chati/kadi za breli, kitabu/kitabu cha breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza mazungumzo yanayoonyesha matumizi ya maneno ya heshima na adabu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake maneno ya heshima na adabu aliyojifunza. | Ni vipi unavyoweza kuonyesha heshima na adabu kwa kutumia maneno? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutazama au kisikiliza maelezo ya picha, michoro na video kuhusu maneno heshima na adabu.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo:mwanafunzi anapotambua baadhi ya maneno ya adabu na heshima na matumizi yake. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu na heshima ipasavyo.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Amani:mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu na heshima anaendeleza amani.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutazama video bila kuzozana.<br>● Uvumilivu: mwanafunzi anapowapa wenzake muda wa kuigiza kuhusu suala lengwa. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuigiza maneno ya heshima na adabu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya maneno ya heshima na adabu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa<br>b) katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kutabiri yanayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>e) kueleza mafunzo yanayotokana na<br>f) kifungu chepesi cha Ufahamu,<br>g) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili uimarisha stadi ya kusoma | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusikiliza au kutazama nyimbo kuhusu majina ya miezi ya mwaka kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusikiliza nyimbo kuhusu majina ya miezi ya mwaka kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutaja majina ya miezi ya mwaka akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuimba nyimbo kuhusu majina ya miezi akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno 55 - 60 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei, Juni, Julai, Agosti, Septemba, Novemba, Disemba)* akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka. | Je, ni vipi unaweza kujifunza kutokana na unachokisoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu chenye fonti ifaayo, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au chati yenye rangi isiyotatiza akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kusikiliza au kusoma maelezo ya picha kwenye kitabu cha breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au kadi za breli akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona atabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia maelezo ya picha kwenye kifungu akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano.<br>• Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake majina ya miezi ya mwaka aliyojifunza ili amtolee maoni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu katika kutabiri kitakachotokea katika hadithi.<br>● Uraia: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi kueleza ujumbe wa kifungu.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali chenye teknolojia saidizi katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi kusoma na kujadili kifungu kuhusu suala lengwa.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka. |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe katika kifungu.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa vya kidijitali darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa vya kidijitali anachotumia kujifunzia. Pia anapowajibikia majukumu aliyopewa wanapofanya maigizo kuhusu miezi ya mwaka.<br>● Haki za kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika shughuli za kusoma kifungu |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka ukakamavu wake unajengeka.<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapozingatia maswala yanayohusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |

**Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**
Chati/ chati za breli za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Hati Nadhifu:** Herufi Ndogo<br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ipasavyo kwenye kifungu,<br>b) kuandika kifungu cha maneno 55-60 akitumia herufi ndogo ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi ndogo. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atazame mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona atambue mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya nukta nundu za herufi ndogo kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua herufi ndogo katika kifungu kilichoko kwenye kitabu, chati, zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nukta nundu za herufi ndogo katika kifungu kilicho kwenye kitabu, chati, zilizo na maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kunakili kifungu | Je, unatambua vipi herufi ndogo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akizingatia matumizi yafaayo ya herufi ndogo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika kifungu chenye maneno 55-60 akizingatia maumbo ya nukta nundu za herufi ndogo zifaazo akizingatia hatua za uandishi (maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake).<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona ashirikiane na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia matumizi yafaayo wa herufi ndogo. Mwanafunzi asiyeona ashirikiane na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia maumbo ya nukta nundu za herufi ndogo yafaayo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuwaonyesha wenzake kifungu alichokiandika akizingatia maumbo ya herufi ndogo ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutambua mfano ufaao wa maumbo ya herufi ndogo au maumbo ya nukta nundu yafaayo

Ushirikiano na mawasiliano : mwanafunzi anapotambua matumizi ya herufi ndogo akiwa na wenzake

**Maadili :**

- Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.Mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.

**Masuala Mtambuko**

- Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za kikundi.
- Udhibiti wa uwezo na kutokea kwa maafa: mwanafunzi anapojifunza shughuli mbalimbali kwenye miezi ya mwaka.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kutumia hati nadhifu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

**Mapendekezo ya nyenzo za Ujifunzaji**

Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | 3.4.1 Matumizi ya **yule** na **wale** *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **yule** na **wale** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya neno **yule** na **wale** katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua matumizi ya **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, kadi maneno zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza, vifaa vya kidijitali vyeneye teknolojia saidizi n.k akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua matumizi ya yule na wale kutoka kwenye chati , kitabu, kadi maneno zilizo na maandishi ya breli na vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusilikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya **yule** na **wale** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi na kujadili | Je, ni vipi unaweza kutunga sentensi ukitumia maneno yule na wale? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | matumizi yake akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma sentensi zilizotumia **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma sentensi zilizotumia **yule** na **wale** kutoka kwenye chati za breli, kitabu vya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia **yule** na **wale** akiwa na wenzake.<br>Mwanafunzi asiyeona aelekezwe moja kwa moja kuigiza vitendo vya watu mbalimbali kwa kutumia **yule** na **wale** akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika sentensi akitumia **yule** na **wale (***k.v Mtoto yule anacheza - watoto wale wanacheza)* na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kujaza nafasi ili | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akamilishe sentensi akitumia **yule** na **wale.** Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kukamilisha sentensi akitumia **yule** na **wale,** kwa kutaja jibu.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake kazi aliyoandika kuhusu matumizi ya **yule** na **wale** ili kufanikisha mawasiliano katika jamii. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia maneno yule na wale.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya yule na wale akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia nafsi ya tatu, umoja na wingi kwa lugha fasaha.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kurejelea watu wa familia yake kwa kutumia maneno yule na wale. |
| **Maadili**<br>● Heshima:mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu, umoja na wingi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kumshirikisha mzazi au mlezi wake katika kurejelea watu wa familia yake kwa kutumia maneno yanayotaja nafsi ya tatu umoja.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu.<br>● Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapowahusisha wengine katika shughuli za kikundi. |

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya yule na wale akishirikiana na wenzake katika kikundi akizingatia suala lengwa.<br>● Masuala ya mazingira: mwanafunzi anaposhiriki katika utunzaji wa mazingira. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya maneno yule na wale aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **4.0 KAZI MBALIMBALI** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora** *Silabi za sauti /**py/**, /**vy**/ na /**sh**/*<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifungu kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | ● Mwanfunzi aliye na upungufu wakuona aelekezwe kutambua silabi za sauti lengwa (/**py/, /vy/, /sh/)** katika matini mbalimbali (k.v kadi maneno, chati, mti maneno zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake, wawiliwili au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua,silabi za sauti lengwa (/py/, /vy/, /sh/) katika matini mbalimbali (k.v kadi maneno, chati, mti maneno zilizo na maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi *(k.v. kupitia programu ya papaya)* kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali vyenye teklnolojia saidizi k.*v. kinasasauti na ununu* akiwa na wenzake kisha azitamke.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza maneno yenye sauti lengwa | Ni vipi utaweza kutamka maneno katika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yakisomwa na mwalimu kisha atambue sauti hizo katika maneno hayo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka maneno yenye sauti ifaavyo akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungfu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kutoka kwa kitabu chenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kutoka kwa kitabu chenye maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anashirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini:mwanafunzi anaposhiriki katika mawasiliano na mzazi au mlezi akitumia maneno ya sauti lengwa.
- Uraia; mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana katika kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshima matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika kutambua silabi za sauti lengwa. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kusoma kifungu chenye maneno ya sauti /***py/,/vy***/ na ***/sh/*** kuhusu swala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli,kadi za maneno/ kadi za breli,mti wa maneno,michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4. 2.1 Kusoma** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sauti lengwa **(*/py/, /vy/, /sh/*)** katika kifungu | 1. Ni vipi utahakikisha |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **kwa Ufasaha:** *Sauti /**py**/, /**vy**/, /**sh**/)*<br><br>(*Vipindi 3*) | a) Kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno kwenye chati, kitabu zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza chenye sauti lengwa kwa kuzingatia maandishi bora akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno kwenye kadi za breli, kitabu kilicho na maandishi ya breli chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 49 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa | umesoma kifungu kwa ufasaha?<br>2. Kwa nini ni muhimu kusoma kwa kuzingatia matamshi bora? |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kuzingatia ishara zifaazo akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu chenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza, kifaa cha kidijtali chenye teknolojia saidizi n.k. akiwa peke yake au na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu chenye maandishi ya breli, kifaa cha kidijtali chenye teknolojia saidizi n.k akiwa peke yake au na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika,kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , na kuchangia kikamilifu katika kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu.<br>● Uraia: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kusoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa.<br>● Kujithamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akitumia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kifungu chenye sauti ***/py/,/vy/*** na ***/sh/.*** |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , kutambua sauti na kusoma kifungu.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu cha maneno yenye sauti lengwa.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Umaskini: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kinachohusu kazi mbalimbali zinazofanywa na jamii ili kupunguza umaskini wao. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | 4.3.1 **Nafasi ya Pambizo katika Uandishi**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya,<br>b) kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 60 akizingatia pambizo na aya,<br>c) kufurahia kuandika kifungu akizingatia aya na pambizo. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya akiwa peke yake au na wenzake au katika kikundi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kifungu na kutambua pambizo na aya kwenye kitabu, chati zilizo na fonti ifaayo na rangi zisizotatiza, kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kifungu na kutambua pambizo na aya ya kitabu cha breli, kutambua kiwango cha seli za breli cha kuruka ili kupata pambizo katika karatasi ya breli wakati wa kuandika.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya kwenye daftari au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuwasomea wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya kwenye karatazi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kuwasomea wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo (*maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea* | Je, kwa nini tuzingatie nafasi za pambizo tunapoandika aya? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *wenzake*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika na amuonyeshe mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ili ampe maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia aya na pambizo akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ipasavyo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake wampe maoni.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.
- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi wakizingatia aya na pambizo.

**Masuala Mtambuko**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia pambizo na aya katika kifaa cha kidijitali.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nafasi ya pambizo katika uandishi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**

Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | 4.4.1 **Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>*(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br><br>b) kuandika sentensi katika umoja na wingi,<br><br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | ● Mwanafuzi aelekezwe kusoma sentensi katika umoja na wingi akiwa peke yake, au na wenzake akizingatia suala lengwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye chati/kadi za breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwa kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushiriki katika mchezo wa kusoma sentensi katika umoja na mwenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika umoja na wingi wa sentensi akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomeee mzazi au mlezi wake sentensi alizoziandika katika umoja na wingi. | 1. Je, utajuaje kama sentensi imeandikwa katika umoja au wingi?<br>2. Ni vipi utakavyotambua umoja na wingi katika sentensi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , kuandika sentensi katika umoja na wingi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapokamilisha sentensi katika umoja na wingi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi sentensi alizoandika katika umoja na wingi. |
| **Maadili**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua sentensi katika umoja na wingi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi katika umoja na wingi.<br>● Heshima**:** mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapoandika umoja na wingi wa sentensi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi zinazohusiana na mapato ya watu na kazi mbalimbali |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya umoja na wingi wa sentensi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **5.0 USALAMA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaowasilishwa katika kifungu,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika kifungu alichosikiliza,<br>c) Kutunga sentensi kutumia msamiati uliotumika kwenye kifungu alichosikiliza,<br>d) kusimulia upya kifungu cha hadithi alichokisikiliza,<br>e) kuchangamkia kutambua msamiatia uliotumika kwenye kifungu alichokisikiliza. | ● Mwanafunzi aelekezwe kujadili ujumbe unaowasilishwa na picha au maelezo ya picha akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu cha maneno 60-65 kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi ili kupata ujumbe unaowasilishwa.<br>● Mwanafunzi alekezwe kutambua msamiati uliotumika katika ufahamu aliousikiliza akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi kwa kutumia msamiati aliousikiliza ukitumika kwenye kifungu.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujibu maswali yanayohusiana na kifungu alichosikiliza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili mambo muhimu katika kifungu | Je, kwa nini ni muhimu kutambua ujumbe unaowakilishwa katika kifungo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alichokisikiliza akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusimulia wenzake upya kifungu alichokisikiliza. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na kuwasiliana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi katika ujifunzaji.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za huduma kwa jamii kwa kusimulia visa vyepesi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anaposimulia upya kifungu alichokisikiliza. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake katika kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunzi vifaa vya kidijitali. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Usalama wa watoto barabarani: mwanafunzi anaposikiliza na kuzungumzia usalama wa watoto barabarani.<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anapozungumza kuhusu haki za watoto. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufahamu wa kusikiliza aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>a) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza au atazame nyimbo kuhusu usalama shuleni kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutaja masuala ya usalama shuleni akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuimba nyimbo kuhusu usalama shuleni akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno 60- 65 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v usalama, hatari, umia, tibu, tahadhari, zahanati, dawa, huduma ya kwanza)* akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi ashirikiane na wenzake kufanya maigizo kuhusu usalama shuleni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha au maelezo ya picha kwenye kitabu, vifaa | 1. Je,ni vipi unaweza kuzingatia mambo yanayotarajiwa kwa usomaji bora?<br>2. Ni kwa nini ni muhimu kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au chati akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au chati yenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza, akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kusikiliza maelezo ya picha kwenye kitabu chenye maandishi ya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi au chati yenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha/maelezo ya picha kwenye kifungu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu kuhusu usalama wake shuleni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika kazi za kikundi wanapojadili ujumbe wa kifungu na kutabiri yatakayotokea katika hadithi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali chenye teknolojia saidizi kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma matini mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa. |
| **Maadili**<br>● Umoja:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadiliana kuhusu ujumbe katika kifungu.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu na kutabiri.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa cha kidijitali darasani. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa jamii: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi na kutoa mchango wake, ukakamavu wake unajengeka.<br>● Usalama mwanafunzi anapotaja maswala ya usalama shuleni.<br>● Udhibiti wa uwezo wa kutokea kwa maafa: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu udhibiti wa uwezo wa kutokea kwa maafa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |

| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji** |
|---|
| Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ Kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | 5.3.1 **Matumizi ya Kiulizi**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya kiulizi katika maandishi,<br>b) kueleza matumizi ya alama ya kiulizi katika maandishi,<br>c) kuandika kifungu cha maneno kati ya 55 - 60 akitumia alama ya kiulizi ipasavyo,<br>d) kufurahia kutumia kiulizi katika maandishi ili kufanikisha mawasiliano. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua alama ya kiulizi kutoka kwenye kitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza, kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi n.k akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona atambue alama ya kiulizi ya breli kutoka kwenye maandishi, kadi za breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi n.k. akiwa na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kutumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika alama ya kiulizi na kuwashirikisha wenzake kuijadili ili kuitolea maoni.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kujadili na wenzake matumizi ya alama ya kiulizi ili kukuza uwezo wa kuitumia ipasavyo.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kunakili ipasavyo kifungu kilichotumia alama ya kiulizi na kujadili na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu | Je, alama ya kiulizi inatumika vipi katika uandishi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | cha maneno kati ya 55 - 60 akizingatia matumizi ya alama ya kiulizi (*akizingatia hatua tano za uandishi; maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu chepesi akizingatia alama ya kiulizi kisha amwonyeshe mzazi au mlezi wake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kuandika katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali : mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia umbo la kiulizi kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Hamu ya ujifunzaji :mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.
- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzakekatika shughuli za kikundi
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia alama kiulizi katika maandish na pia anapotumia vifaa vya kidijitali.

**Masuala Mtambuko**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoelekezwa kutangamana na mitandao ya kijamii kwa njia salama.
- Kuokoa pesa: mwanafunzi  anapoandika kifungu chepesi kuhusu uokoaji wa pesa akizingatia matumizi ya kiulizi.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya alama ya kiulizi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji** |
| --- |
| Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **5.4 Sarufi** | 5.4.4. **Matumizi ya -ake na -ao** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-ake** na **-ao** katika mawasiliano,<br>b) kutumia **-ake** na **-ao** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **- ake** na **-ao** kufanikisha mawasiliano | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua matumizi ya **-ake** na **–ao** kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno au chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua matumizi ya **-ake** na **–ao** kutoka kwenye kadi za breli, mti maneno, kapu maneno au chati zilizo na maandishi ya breli akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia –**ake** na –**ao** kutoka kwa mgeni mwalikwa, mwalimu au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu kilichotumia **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza matumizi ya **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake katika kikundi kwa kutumia vitu anavyomiliki k.m. *kiti chake – viti vyao.*<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia **-ak**e na **-ao** na azijadili na mwenzake ili kuzitolea maoni.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe | Je, –ake na -ao hutumiwa vipi katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **-ake** na **-ao.** Mwanafunzi asiyeona atambue jibu la kukamilisha sentensi zilizotumia **-ake** na**-ao.**<br>● Mwanafunzi amtungie mzazi au mlezi sentensi zilizo na **-ake** na **-ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapomtungia mwenzake katika kikundi sentensi akitumia **-ake** na **-ao**.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutumia **-ake** na **-ao** kurejelea vitu mbalimbali nyumbani.
- Ujuzi wa kidijitali; mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya **-ake** na **-ao.**
- Ubunifu: mwanafunzi anapomtungia mwenzake katika kikundi sentensi kwa kutumia **-ake** na **-ao**.

**Maadili**

- Heshima mwanafunzi anapoheshimu michango ya wenzake.
- Uwajibikaji : mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na anapotumia vifaa vya kidijitali.
- Umoja:mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Tamaduni hasi za kijamii : mwanafunzi anapotumia **-ake** na **-ao,**katika sentensi akizingatia suala la tamaduni hasi za kijamii.
- Mahusiano na wenzake : mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **-ake** na **-ao**.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya **-ake** na **- ao** aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo

| |
|---|
| la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/kadi za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **6.0 USAFI WA MAZINGIRA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora:** *silabi za sauti* ***/dh/, /th/*** *na* ***/ch/***<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifungu kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini, | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua silabi za sauti lengwa **(/dh/, /th/ na /ch/)** katika kitabu , kadi maneno, chati ,mti maneno, zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akiwa peke yake au na wenzake.<br>Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua silabi za sa sauti lengwa ***(/dh/, /th/ na /ch/)*** katika kitabu, chati kadi zilizo na maandishi ya breli na vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. | 1. Je, ni vipi matamshi bora hufanikisha mawasiliano?<br>2. Je, kwa nini matamshi bora ni muhimu katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuambatanisha silabi na kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi asikilize sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutambua sauti lengwa akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa na kusikiliza kwa makini pamoja na wenzake ili kutathmini matamshi. | |

| Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa |
| --- |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa ,.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika mawasiliano na mzazi au mlezi akitumia maneno ya sauti lengwa.<br>● Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi. |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutamka maneno ya silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshima matamshi yawenzake katika shughuli za vikundi.<br>● Amani:mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu anapotambua silabi za sauti lengwa. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi kinachohusu usafi wa mazingira akizingatia silabi za sauti lengwa na matamshi bora.<br>● Usalama mtandaoni : mwanafunzi anapotambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifaa cha kidijitali azingatie |

| |
|---|
| hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha:** *Sauti* ***/dh/, /th/*** *na* ***/ch/*** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sauti lengwa ***(/dh/, /th/ na /ch/)*** katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake. | Ili kueleweka na kusikika unastahili kusoma vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (*Vipindi 3*) | matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 51 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , na kuchangia katika kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi bila ubaguzi.
- Kujithamini : mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu cha maneno kuhusu suala lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali : mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali chenye teknolojia saidizi kusoma hadithi kwa kutumia matamshi bora.
- Hamu ya ujifunzaji : mwanafunzi anaposoma matini mbalimbali kuimarisha stadi ya kusoma.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa.<br>● Upendo: mwanafunzi anawashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali kusoma hadithi.<br>● Uwajibikaji**:** mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni zifaazo za usomaji. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za ujifunzaji**<br>Chati/chatiza breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Imla**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotamkwa kwenye imla ili kuyaandika ipasavyo,<br>b) kuandika kifungu cha maneno 55-60 yanayotamkwa kwenye imla akizingatia kanuni za uandishi zifaazo,<br>c) kuchangamkia kuandika kifungu akitumia maneno yanayotamkwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za uandishi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno yanayotamkwa yakizingatia suala na sauti /**dh/, /th/** na **/ch/** na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutoka kwenye kitabu, chati, kapu la maneno yaliyo na maneno yenye fonti zifaazo na rangi zisizotatiza akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno yanayotamkwa yakizingatia suala na sauti /**dh/, /th/** na **/ch/** na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kutoka kwenye kitabu cha breli, chati ya breli, kapu la maneno ya breli akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kwa makini maneno yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijital*i* chenye teknolojia saidizi ili kuyaandika ipasavyo.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu cha maneno 55 - 60 yatakayotamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k. akizingatia kanuni zifaazo | 1. Ni kwa nini ni muhimu kuzingatia kanuni za uandishi ipasavyo?<br>2. Imla huandikwaje? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | za uandishi (*k.m. Matumizi ya herufi kubwa na ndogo, tahajia, nafasi baina ya maneno nk*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na wenzake kifungu alichokiandika ili kukitathmini. Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia kanuni za uandishi zifaazo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano; mwanafunzi anapowaeleza wenzake maneno katika kifungu cha imla.
- Ujuzi wa kidijitali; mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha imla akitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Hamu ya ujifunzaji; mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuandika maneno na kifungu cha imla.
- Kujiamini; mwanafunzi anapojifunza kutambua maneno yenye sauti lengwa na kujirekebisha.

**Maadili**

- Upendo mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Heshima mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji wa imla.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno yatakayotamkwa na mwalimu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za maandishi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya imla aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/kadi za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **6.4**<br>**Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya - eupe, -eusi, - ekundu**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yenye - **eupe, -eusi na - ekundu** ili kuyatumia ipasavyo katika mawasiliano,<br>b) kutumia**-eupe, - eusi, -ekundu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia**-eupe, -eusi, - ekundu** katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua maneno yenye **-eupe, - eusi, - ekundu** kwa kurejelea vitu halisi katika mazingira yake, kwenye kitabu, chati zilizo na maneno yenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. n.k. akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua maneno yenye **-eupe, - eusi, -ekundu** kwa kurejelea vitu halisi katika mazingira yake, kwenye kitabu cha breli, chati ya breli, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi. n.k. akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza maelezo kuhusu matumizi ya, **- eupe, -eusi, -ekundu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia maneno yenye **- eupe, -eusi, -ekundu** akiwa peke | Je, kwa nini ni muhimu kutambua vitu na rangi yake? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zinazotumia maneno yenye **-eupe, -eusi, - ekundu** akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zenye matumizi ya - **eupe, -eusi, -ekundu** akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga akitumia vifaa halisi vyenye rangi lengwa vinavyopatikana katika mazingira yake. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia -eupe, -eusi, -ekundu akiwa na wenzake kukamilisha sentensi .<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali vyenye teknolojia saidizi kusikiliza matumizi ya -eupe, -eusi, - ekundu.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anamsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga akitumia -eupe, -eusi, -ekundu.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anatumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** kutunga sentensi. |
| **Maadili**<br>● Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua maneno yenye -eupe, -eusi na -ekundu ipasavyo. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano kwa kijamii: mwanafunzi anaposikiliza maelezo kuhusu matumizi ya, **-eupe, -eusi, -ekundu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| 7.0 DUKANI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi yanapotolewa darasani,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani,<br>c) kufururahia kuzingatia maagizo katika maisha ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua aina mbalimbali za maagizo kwenye kitabu, chati zenye maneno yenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua aina mbalimbali za maagizo kwenye kitabu cha breli, chati za breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake katika kutoa na kufuata maagizo mepesi kama vile (hatua tatu) k.m. *simama uende uufungue mlango.*<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutazama matukio ya video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwa kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusikiliza maelezo ya matukio ya video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwa kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa | Ni kwa nini maagizo huwa muhimu katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushiriki katika mjadala wa maagizo yafaayo na yasiyofaa kufuatwa akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuimba nyimbo na kukariri mashairi mepesi yanayohusu maagizo akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza maagizo mepesi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi amwimbie mzazi au mlezi wake wimbo unaoashiria maagizo ili atoe maoni yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika masimulizi na wenzake ya kufuata na kutofuata maagizo.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa maoni katika majadiliano kuhusu jinsi ya kufuata maagizo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kujifunzia.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposhiriki katika kuimba nyimbo na pia kukariri mashairi kuhusu maagizo.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala wa maagizo yanayofaa na yasiyofaa kufuatwa akiwa na wenzake.

**Maadili**

- Amani: mwanafunzi anapofanya kazi katika kikundi na wenzake kwa utulivu.
- Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake kwa upole na kuelewana.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Udhibiti,kuzuia uigizaji wa silaha ndogondogo na usalama wa mtandaoni : mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za jinsi ya kufuata maagizo yanayolenga suala lengwa.<br>● Elimu ya kifedha : mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo juu ya matumizi ya pesa dukani. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kutoa na kufuata maagizo aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/kadi za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **7.2. Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** (*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa | ● Mwanafunzi aelekezwe kutaja majina ya vitu vinavyopatikana dukani akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno 65 - 70 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v duka, bidhaa, pesa, uza, nunua, chenji, mteja, muuzaji)* akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake. | Je, unatambua vipi ujumbe wa kifungu cha hadithi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | ● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake kufanya maigizo baina ya muuzaji na mnunuzi.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona atabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu chenye fonti inayofaa na rangi isiyotatiza akiwa na wenzake.<br>Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kusikiliza maelezo ya picha kwenye kitabu chenye maandishi ya breli akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi akizingatia picha au maelezo ya picha akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuthibitisha utabiri wake kuhusu kifungu baada ya kukisoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu wanapotabiri na kujadili ujumbe katika kifungu.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa na kuthibitisha utabiri wake kuhusu kitakachotokea katika hadithi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali vyenye teknolojia saidizi kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi wake kusikiliza kifungu kuhusu suala lengwa.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili picha na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.<br>● Haki za kijamii mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji mwanafunzi anapotabiri kilichotokea katika kifungu alichokisoma.<br>● Amani mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo ya mnunuzi na mwuzaji. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapozingatia masuala yanayohusiana na shughuli za dukani.dukanimwanafunzi anapotambua aina za fedha kutokana na suala lengwa.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapotambua aina za fedha kutokana na suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Uandishi wa Insha** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa kisa (k.v.wahusika, ujumbe, muundo n.k).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kisa kikitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au | Je, unatambua vipi mambo muhimu katika uandishi wa insha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (*Vipindi 3*) | ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika kisa cha kati ya maneno 85-90 kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusoma kielelezo cha insha kwenye kitabu, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusoma kielelezo cha insha kwenye kitabu, chati zilizo na maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua kanuni muhimu za uandishi (*k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.*).<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na ajadili na wenzake; kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu kisha amwonyeshe mzazi au mlezi wake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kujadili na wenzake kutambua vipengele vya uandishi wa insha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuandika insha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu.
- Uraia: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za uhariri.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Upendo mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mahusiano ya kijamii mwanafunzi anapowathamini wenzake na kushirikiana katika shughuli za uhariri.<br>● Aina za fedha mwanafunzi anapotambua aina za fedha kutokana na suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa insha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, kadi maneno/ kadi za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Mapendekezo ya Shughuli ya Ujifunzaji** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **7.4** | **7.4.1** | Kufikia mwisho wa mada | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe | Je, unatambua |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Sarufi** | **Ukanushaji wa nafsi ya tatu**<br><br>(*Vipindi 3*) | ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi,<br>b) kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika mawasiliano ya kila siku. | kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno, chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidiziakiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno, chati zilizo na maandishi ya breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi kwa kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia nafsi ya tatu umoja, wingi na ukanushaji wake (*kwa mfano: yeye anaandika, yeye haandiki).*<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza matumizi ya nafsi ya tatu umoja, wingi na ukanushaji akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi sentensi za nafsi ya tatu umoja na wingi zilizokanushwa kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. | vipi ukanushaji wa nafasi ya tatu umoja na wingi katika sentensi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu umoja akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotungia mwenzake sentensi katika kikundi akitumia ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu matumizi ya nafsi ya tatu umoja.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kutumia ukanusho wa nafsi ya tatu umoja |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu matumizi ya nafsi ya tatu umoja.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu umoja katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za ukanushaji.<br>● Masuala ya afya ya akili: mwanafunzi anapotumia ukanusho katika sentensi zinazolenga masuala ya afyaya akili. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ukanushaji aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/kadi za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa |

| |
|---|
| **8.0 NDEGE NIMPENDAYE** |

| Mada | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | 8.1.1 **Matamshi Bora:** *Silabi za sauti* ***/mbw/,/nd/*** *na* ***/ny/***<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua silabi za sauti lengwa (/***mbw/,/nd/, /ny***/) katika kadi maneno, chati, mti maneno zilizo na maneno yenye fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua silabi za sauti lengwa (/**mbw/,/nd/, /ny**/) katika kadi, chati zilizo na maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutambua sauti lengwa akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka maneno aliyosikiliza yenye sauti lengwa atamke na mwalimu na mwishowe atamke akiwa peke yake au | Je, matamshi bora hukuzwa kwa njia gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu cha hadithi na kutambua sauti lengwa.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kwa sauti kifungu kilicho na sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua vyenye teknolojia saidizi na kutamka maneno yenye sauti lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli mbalimbali ili kuboresha matamshi yake.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na azisikilize na wenzake ili kutathmini matamshi.<br>● Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka silabi za sauti lengwa akitumia nyenzo mbalimbali. |
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana , kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia sadizi katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wenzake katika matumizi ya vifaa vya kidijitali. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposoma kifungu kilicho na sauti ***mbw, nd*** na ***ny*** kuhusu suala lengwa kwa ufasaha na matamshi bora. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/kadi za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufasaha:** *Sauti /mbw/, /nd/ na /ny/*<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | • Mwanafunzi aelekezwe kutambua sauti lengwa (*/mbw/, /nd/, /ny/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa peke yake au na wenzake .<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 53 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akiwa peke yake au na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa peke yake au na | 1. Je, ni vipi unaweza kusoma kwa ufasaha?<br>2. Ni kwa nini ni muhimu kusoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mwenzake, mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo kwa ufasaha. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya kazi ,.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali chenye teknolojia saidizi kusoma hadithi akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika,kasi ifaayo na ishara zifaazo..
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake na kusoma kifungu chepesi kwa ufasaha.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi kujadiliana.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti /***mbw/, /nd/*na */ny***/ kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika,kasi ifaayo na ishara zifaazo .

**Uhusiano na Masomo Mengine;**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

| Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji |
|---|
| Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | 8.3.1 **Tahajia**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi za maneno katika insha,<br>b) kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>c) kufurahia kutumia tahajia sahihi katika maandishi. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua tahajia sahihi za maneno katika uandishi wa insha kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua nukta nundu mwafaka za maneno katika uandishi wa insha kwenye kitabu cha breli ua kifaa cha kidijitali chenye teknolojia sidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kushirikiana na wenzake kujadili kuhusu tahajia sahihi ya maneno katika kifungu kitabuni, kwenye kitabu cha breli au kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno katika uandishi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kurekebisha insha akizingatia tahajia za maneno.<br>● Mwanafunzi amsomee mwenzake, mzazi au mlezi insha aliyoiandika kwa kuzingatia tahajia za maneno. | Kwa nini unafaa kutumia tahajia ipasavyo katika maandishi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujifunza kutumia tahajia ifaavyo katika mawasiliano.<br>● Ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika makundi kutambua tahajia sahihi za maneno katika insha.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kujifunza tahajia sahihi za maneno katika insha.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji wa tahajia sahihi za maneno katika insha. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao katika shughuli za vikundi..<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuhusu tahajia. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapojifunza kuandika insha kuhusu ndege nimpendaye akizingatia kanuni za uandishi na tahajia sahihi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya tahajia aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **8.4.Sarufi** | 8.4.1 **Matumizi ya maneno Hili na Haya** <br> *(Vipindi 3)* | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze: <br> a) kutambua matumizi ya maneno **hili** na **haya** katika kifungu, <br> b) kutumia maneno **hili** na **haya** katika kifungu ili kuboresha mawasiliano, <br> c) kuchangamkia matumizi ya **hili** na **haya** katika mawasiliano. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua matumizi ya maneno **hili** na **haya** *(jicho hili – macho haya, jino hili – meno haya n.k.)* katika kifungu kwenye chati, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua matumizi ya maneno **hili** na **haya** *(jicho hili – macho haya, jino hili – meno haya n.k.)* katika kifungu kwenye chati ya breli yenye maandishi yenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza, vyombo vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi n.k akiwa peke yake au na wenzake. <br> • Mwanafunzi aelekezwe kusoma sentensi zinazoonyesha matumizi ya **hili** na **haya** katika kifungu akiwa peke yake au na wenziwe. <br> • Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi akitumia maneno **hili** na **haya** akiwa peke yake au na wenzake. <br> • Mwanafunzi aelekezwe kuandika kifungu akitumia maneno **hili** na **haya** na kujadili | Ni vipi **hili** na **haya** hutofautiana kataka matumizi kwa sentensi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na wenzake ili kukitolea maoni.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu alichokitunga ili akitolee Maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojenga msingi wa kujifunza zaidi kuhusu maneno hili na haya.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia matumizi ya hili na haya.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotumia **hili** na **haya** kurejelea vitu katika mazingira yake.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , kutunga sentensi akitumia hili na haya ipasavyo
- Amani: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali na wenzake ili kutambua na kutunga sentensi akitumia **hili** na **haya** kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kutambua matumizi ya hili na haya kutoka kwenye nyenzo mbalimbali na kutumia kuonyesha vifaa mbalimbali katika jamii.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya vivumishi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**

Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| **9.0 SOKONI** | | | | |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala lengwa linalozungumziwa,<br>b) kuzingatia matamshi bora katika mazungumzo,<br>c) kujieleza kwa ufasaha kuhusu suala lengwa,<br>d) kutumia ishara zifaazo katika mazungumzo,<br>e) Kuchangamkia mazungumzo katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua suala lengwa linalozungumziwa kupitia kwa picha kutoka kwenye kitabu, chati zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia sidizi pamoja na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua suala lengwa linalozungumziwa kupitia maelezo ya picha, kutoka kwenye kitabu, chati zilizo na maandishi ya breli na vifaa vya kidijitali vyenye technolojia saidizi pamoja na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuchukua muda wa kufikiri kuhusu suala la kuzungumzia.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kupanga mawazo yake kuhusu suala lengwa na kuandaa hoja za kuzungumzia.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka maneno kwa kuzingatia matamshi yafaayo ya sauti mbalimbali. | 1. Je, mtu hufaidika vipi kutokana na mazungumzo?<br>2. Kwa nini ni muhimu kuzingatia matamshi bora katika mazungumzo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Mwanafunzi aelekezwe kueleza habari ambayo zinaleta maana na zenye kufuatana vizuri.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kupandisha na kushusha sauti panapohitajika.<br>• Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutumia ishara mbalimbali zinazohusiana na maelezo yake kuhusu suala lengwa. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutumia kiimbo/toni mbalimbali zinazohusiana na maelezo yake kuhusu suala lengwa.<br>• Mwanafunzi azungumze na mzazi au mlezi wake akizingatia suala lengwa ili aimarishe mawasiliano. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na wenzake katika kikundi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa ubashiri kutoka kwa picha.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali chenye teknolojia saidizi kusikiliza mazungumzo.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo ya kila siku ili kuimarisha mawasiliano.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapowaeleza wenzake kisa kuhusu suala lengwa. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali na nyenzo nyinginezo anazotumia kujifunzia.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowasikiliza wenzake darasani na kuheshimu maoni yao. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Umasikini: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu shughuli za sokoni zinazolenga umasikini.<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo kuhusu utumiaji wa pesa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya stadi za mazungumzo aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>**C**hati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **9.2. Kusoma** | 9.2.1 **Kusoma kwa ufahamu** (***Vipindi 3***) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi,<br>c) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi akitumia nyenzo kama vile chati, kadi maneno, mti maneno zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi. Mwanafunzi aelekezwe kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi akitumia nyenzo kama vile chati, kadi maneno, mti maneno zilizo na maandishi ya breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno 70- 75 na kutambua msamiati wa suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● Mwanafunzi aelekezwe kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake. | Je, kwa nini ni muhimu kutambua mambo yanayozingatiwa katika kusoma ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi wake na kujadili ujumbe katika kifungu kuhusu suala lengwa. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu katika kutabiri na kueleza ujumbe katika kifungu.<br>● Uraia: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali chenye teknolojia saidizi katika kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anpomshirikisha mzazi au mlezi kusoma na kujadili ujumbe katika kifungu kuhusu suala lengwa. |
| ● **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe na kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu darasani.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa cha kidijitali darasani. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anapotambua msamiati kuhusu masuala ya kijinsia .<br>● Elimu ya fedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu aina za fedha. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya |

| |
|---|
| kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | 9.3.1 **Insha ya Masimulizi**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia uandishi wa insha ya masimulizi ili kuimarisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza masimulizi yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya masimulizi kutoka kwenye masimulizi aliyosikiliza.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma insha kielelezo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuhusu insha ya masimulizi akiwa na wenzake. Mwanafunzi aelekezwe kusoma insha kielelezo kwenye kitabu cha breli, chati za breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi kuhusu insha ya masimulizi akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua mambo muhimu katika uandishi | Je, kanuni za uandishi husaidia vipi katika uandishi wa insha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | k.v. mwandiko nadhifu, maudhui, mtiririko katika kielelezo cha insha aliyosoma.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na ajadili na wenzake; kisa hiki kifuate hatua za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kisa kifupi kuhusu suala lengwa ili akitolee maoni | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kuandika katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu cha kusimulia akitumia kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi katika shughuli ya kuandika.
- Uwazaji wa kina: mwanafunzi anapotambua mambo yanayotakikana katika uandishi wa insha fupi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana nawenzake katika shughuli za kikundi kutambua msamiati wa suala lengwa na kujadili ujumbe ma mafunzo ya kufungu cha ufahamu.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali

**Masuala Mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya masimulizi inayolenga maswala ya tabia nchi.
- Matumizi ya dawa za kulevya: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu matumizi ya dawa za kulevya.

| |
|---|
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa insha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Matumizi ya juu ya ndani ya na, mbele ya**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu,<br>b) kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika mawasiliano ya kila siku. | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika matini andishi au simulizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kutoka kwa mgeni mwalikwa, mwalimu au vifaa vya kidijitali chenye teknolojia saidizi na kutambua matumizi ya maneno haya akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu kilichotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujadili na mwenzake matumizi ya **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu ili kukitolea maoni.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake. | Je, juu ya, ndani ya, na mbele ya, hutumika vipi kurejelea kitu/ mtu aliye mahali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuigiza matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake kwa kutumia vitu vinavyopatikana katika mazingira yake k.m; *Mboga iko ndani ya gunia,Vitabu viko juu ya rafu, Kitabu kiko ndani ya mkoba, Gari liko mbele ya duka,*<br>● Mwanafunzi amtungie mzazi au mlezi wake sentensi kwa kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kwa kuzingatia vitu katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawisiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia juu ya, ndani ya na mbele ya
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo na vileviile anapofanya zoezi kwa kutumia tarakilishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowatungia wenzake sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya.**

**Maadili**

- Heshima: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi huku akiyaheshimu maoni na michango ya wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi na pia anapotangamana na vifaa vya kidijitali.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko:**

- Kupambana na ufundishaji wa misimamo mikali, unyanyazaji uliokithiri na ugaidi: mwanafunzi anapotumia juu ya, ndani ya na mbele ya katika sentensi zinazohusu uzuiaji wa ugaidi.
- Haki za watoto: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake kujieleza akitumia suala lengwa.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoigiza uuzaji na ununuzi katika suala lengwa akitumia juu ya,ndani ya na mbele ya.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya vihusishi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**

Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi, mgeni mwalikwa

**10.0 TEKNOLOJIA**

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

<table>
<tr>
<td>10.1<br>Kusikiliza na Kuzungumza</td>
<td>10.1.1<br><br>Matamshi Bora:<br>Sauti /mb/,<br>/nz/ na /tw/<br><br>(Vipindi 3)</td>
<td>Kufikia mwisho wa Mada Ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno na kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye silabi za sauti lengwa ili kufanikisha mawasiliano,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano.</td>
<td>● Mwanafunzi aliye na upungufu wakuona aelekezwe kutambua silabi za sauti lengwa (/mb/, /nz/, /tw/) katika kitabu, kadi maneno, mti maneno na chati zilizo na fonti zifaazo na rangi zisizotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua silabi za sauti lengwa (/mb/, /nz/, /tw/) katika kitabu, kadi , chati, mti maneno zilizo na maandishi ya breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kusikiliza na atambue silabi za sauti lengwa (/mb/, /nz/, /tw/) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno zenye maandishi yenye fonti ifaayo na rangi isiyotatiza au vifaa vya kidijitali akiwa peke yake, au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kusikiliza na atambue silabi za sauti lengwa (/mb/, /nz/, /tw/) katika kitabu cha breli, kadi za breli, chati za breli, mti maneno au vifaa vya kidijitali akiwa peke yake, au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza</td>
<td>1. Je, unaweza kufanikisha vipi utamkaji wa sauti /mb/, /nz/ na /tw/?<br>2. Je, matamshi bora hufanikisha mawasiliano vipi?</td>
</tr>
</table>

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa (*km mboga, mbuzi, mbao, nzuri, mwanafunzi, twende, kutwa, katwa, nk*) akishirikiana na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa akisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi kifungu kifupi kwa kuzingatia silabi za | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sauti lengwa kwa matamshi bora. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi wanashirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu chenye maneno ya sauti lengwa ili watathmini na wenzake.

| |
|---|
| **Maadili**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima**:** mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakisikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa. |
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoambatanisha silabi na kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa kuhusu teknolojia na wenzake kutoka maeneo mbalimbali.<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua silabi za sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali azingatie hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotarajiwa | Mapendekezo ya Shughuli za Ujifunzaji | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **10.2 Kusoma** | 10.2.1 **Kusoma kwa Ufasaha:** *Sauti* ***/mb/,/nz/*** *na* ***/tw/***<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha | ● Mwanafunzi aelekezwe kutambua sauti lengwa **(/mb/, /nz/, /tw/)** katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno yenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (maneno 55 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi) akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi amsomee mwenzake, mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | 1. Je, kwa nini ni muhimu kuweza kusoma maneno yenye sauti **/mb/, /nz/, /tw/?**<br>2. Kwa nini ni muhimu kusoma kifungu kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ili kufanikisha mawasiliano. | | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kusoma ,.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu chenye sauti lengwa darasani.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani .
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali

**Masuala Mtambuko:**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali inayohusu suala lengwa,awajibike na akizingatia hatua za kiusalama.*k.v. kutowasiliana na watu asiowajua.*
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa pamoja na wenzake kutoka jamii mbalimbali akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo, sauti inayosikika na ishara zifaazo.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

**Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**

Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/ Kadi za breli, mti maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotrajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vinavyozingatiwa katika insha ya maelezo ili kujiandaa kuandika,<br>b) Kuandika insha ya maelezo kati ya maneno 85-90 kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia kuandika insha ya maelezo ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano. | ● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo (km, wahusika, ujumbe, muundo nk) kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali chenye teknoloji saidizi *a*kiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo (km, wahusika, ujumbe, muundo nk) kwenye kitabu cha breli au kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi *a*kiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza maelezo yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kusoma insha kielelezo kuhusu maelezo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutambua kanuni za uandishi katika uandishi k.v. mwandiko nadhifu, mtiririko n.k. akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kuandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa akizingatia | 1. Je, ni vipi unatumia kikomo katika maandishi?<br>2. Je, unatumia maneno ya aina gani unapotoa maelezo kuhusu kitu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | hatua tano za uadishi (maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake) na kuijadili na wenzake ili waitolee maoni.<br>● Mwanafunzi amsomee mzazi au mlezi insha ya maelezo aliyoandika. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , na kuchangia kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia matumizi yafaayo ya kikomo kwenye kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika.

**Maadili**

- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa akizingatia hatua za uandishi na hatua za kiusalama.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana uadhishi wa insha aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language.

| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji** |
|---|
| Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno/kadi za breli, mti wa maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum ya Ujifunzaji Yanayotrajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya vitendo**<br><br>(*Vipindi 3*) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo katika matini,<br>b) kutumia vinyume vya vitendo ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | • Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kutambua vinyume vya vitendo (k.v. fungua- funga, keti- simama, ezeka -ezua, twika- tua) katika kifungu kwenye chati, kitabu zilizo na fonti zinazofaa na rangi zisizotatiza au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe kutambua vinyume vya vitendo (k.v. fungua- funga, keti- simama, ezeka -ezua, twika- tua) katika kifungu kwenye chati za breli, kitabu vya breli au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusikiliza kifungu chenye vinyume vya vitendo kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi akiwa peke yake au na wenzake.<br>• Mwanafunzi aelekezwe kusoma vinyume vya | Je, unatambua vipi vinyume vya vitendo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vitendo katika kifungu akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kukamilisha sentensi akitumia vinyume vya vitendo akiwa peke yake au na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kutunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni.<br>● Mwanafunzi aliye na upungufu wa kuona aelekezwe kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake. Mwanafunzi asiyeona aelekezwe moja kwa moja kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake.<br>● Mwanafunzi aelekezwe kumtajia mzazi au mlezi vinyume vya maneno alivyojifunza darasani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake , na kuchangia kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia matumizi yafaayo ya kikomo kwenye kifaa cha kidijitali chenye teknolojia saidizi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika.

**Maadili**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa ,.
- Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi pamoja na wenzake kikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake kutoka jamii tofafauti tofauti bila ubaguzi.<br>● Usalama mtandano: mwanafunzi anapotambua vinyume vya vitendo katika kifungu kutoka kwenye kifaa cha kidijitali,azingatie hatua zifaazo za usalama k.v kuwajibika anaposakura tovuti. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume vya vitendo aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language. |
| **Mapendekezo ya Nyenzo za Ujifunzaji**<br>Chati/chati za breli, vitabu/vitabu vya breli, kadi za maneno, mti maneno, michoro/maelezo ya michoro, vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

**MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA**

**MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali Na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora. (*vokali za Kiswahili, konsonanti za Kiswahili;*/***py/,/vy/,/sh/,/mb/,/nz/,/tw/ /dh/,/th/,/ch/,/mbw/,/nd/,ny/***) | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti kati ya 10-12 kikamilifu. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti kati ya 7-9 kikamilifu. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti kati ya 4-6 kikamilifu. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti kati ya 1-3 kikamilifu. |

| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha. *(kwa kutumia maneno ya heshima na adabu na mazungumzo ya kimuktadha)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno ya heshima na adabu na katika mazungumzo mbalimbali kwa uketo. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno ya heshima na adabu na katika mazungumzo mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia baadhi ya maneno ya heshima na adabu na katika baadhi ya mazungumzo. | Anazungumza na kujieleza kwa akitumia baadhi ya maneno ya heshima na adabu na katika baadhi ya mazungumzo kwa kutatizika. |
| Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo. (*maamkuzi, maagano,kifungu na maagizo*) | Anasikiliza na kujibu maamkuzi, maagano na kifungu na kutoa na kufuata maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa urahisi. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi, maagano na kifungu na kutoa na kufuata maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi, maagano na kifungu, na kutoa na kufuata baadhi ya maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi maagano na kifungu, na kutoa na kufuata baadhi ya maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa kutatizika. |

**MADA: KUSOMA**

| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kusoma kwa ufahamu – kifungu *( ujumbe, matumizi ya msamiati mwafaka, kutabiri,kueleza mafunzo)* | Anasoma vifungu na kutambua ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo kwa | Anasoma vifungu na kutambua ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo. | Anasoma vifungu na kutambua baadhi ya ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo. | Anasoma vifungu na kutambua baadhi ya ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | utendeti. | | | kwa kiasi. |
| Kuweza kusoma kwa ufasaha. (*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti*, *kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 4 vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele 3 vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele 2 vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya kipengele 1 cha kusoma kwa ufasaha. |

**MADA: KUANDIKA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidi matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kuandika kwa hati nzuri/nadhifu ya breli, kutenganisha herufi ipasavyo na kuacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika kwa hati nadhifu/hati nadhifu ya breli unaosomeka, anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni kwa wepesi. | Anaandika kwa hati nadhifu/hati nadhifu ya breli unaosomeka, anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika kwa hati usio nadhifu/hati nadhifu ya breli lakini unaosomeka, anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika hati/hati nadhifu ya breli isiyosomeka kwa urahisi, anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno na pambizoni kwa kuongozwa. |
| Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha. ( *masimulizi, maelezo* ) kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 4 vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele 3 vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele 2 vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya kipengele 1 kifaaacho cha uandishi. |
| Kuweza kuzingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia alama 6 za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha kwa utendeti. | Anazingatia alama kati ya 4-5 za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia alama kati ya 2-3 za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia baadhi ya alama 1 ya uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. |

**MADA: SARUFI**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuweza kutambua na kutumia maneno mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. *(yeye,wao , huyo yule,wale,hili,haya, -ake, -ao, eupe, -eusi, -ekundu, juu ya, ndani ya, mbele ya)* | Anatambua na kutumia maneno 4 mbalimbali katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia maneno 3 mbalimbali katika matini. | Anatambua na kutumia maneno 2 katika matini. | Anatambua na kutumia neno 1 katika matini. |
| Kuweza kutambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno. *(Vinyume vya vitenzi)* | Anatambua vinyume vya maneno 7 na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya maneno kati ya 5-6 na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya maneno kati ya 3-4 na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya maneno kati ya 1-2 na kuvitumia katika neno. |
| Kuweza kutambua na kutumia umoja na wingi wa maneno, vifungu vya maneno na sentensi. | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa maneno 4. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa maneno 3. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa maneno 2. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa neno 1. |
| Kuweza kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. *( ukanushaji wa nafsi ya tatu, vinyume vya vitenzi)* | Anatambua maneno 7 yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi kwa wepesi. | Anatambua maneno kati ya 5-6 yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. | Anatambua maneno kati ya 3-4 yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. | Anatambua maneno kati ya 1-2 yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. |

**KIAMBATISHO I: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL)**

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya CSL ni kuambatanisha dhana zilizofunzwa darasani katika masomo mbalimbali na tajriba za maisha halisi ya mwanafunzi aliye na changamoto za kuona. Huwawezesha wanafunzi walio na changamoto za kuonakuona jinsi mambo waliyojifunza yanavyohusiana na maisha ya kila siku. CSL huwa katika somo la *Environmental Activities*. Mwalimu darasani anatarajiwa kutambua na kuwaelekeza wanafunzi kutekeleza shughuli ya CSL ya darasa zima na jumuishi inayofaa kulingana na umri wa wanafunzi ndani ya shule. Usalama wa wanafunzi walio na changamoto za kuonaunafaa utiliwe maanani wakati wa kuchagua shughuli hii. Zifuatazo ni hatua za shughuli ya CSL jumuishi ambayo inafaa itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula wa shule.

| **Hatua za utekelezaji wa CSL jumuishi** |
|---|
| 1. **Maandalizi**<br>● Amua shughuli itakayotekelezwa na wanafunzi.<br>● Tambua umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo mahususi kwa shughuli ya CSL.<br>● Tambua nyenzo hitajika kwa shughuli hiyo (vifaa vinavyopatikana karibu).<br>● Panga shughuli hiyo itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula (weka tarehe na saa ya shughuli).<br>● Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule, walimu na wadau wengine katika jamii ya shule.<br>● Tambua na ukuze vifaa vya kutathminia. |
| 2. **Utekelezaji wa shughuli ya CSL**<br>● Wapatie wanafunzi majukumu.<br>● Hakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika shughuli hii.<br>● Watazame wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya CSL na uweke rekodi ya matokeo.<br>● Tumia kifaa kifaacho chenye teknolojia saidizi cha tathmini kutathmini mchakato wa shughuli na matokeo (tathmini kazi ya wanafunzi kutoka mwanzo hadi mwisho).<br>● Tathmini umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo. |
| 3. **Utafakuri wa shughuli ya CSL**<br>Kuwa na muda wa tathmini binafsi na wanafunzi kuhusu shughuli waliyotekeleza ya CSL jumuishi kwa kujadili yafuatayo:<br>● Ni nini kilifanyika vyema na kwa nini.<br>● Ni nini ambacho hakikufanyika vizuri na kwa nini.<br>● Ni nini kinachoweza kufanywa kwa njia tofauti wakati ujao.<br>● Ni nini wanafunzi walijifunza. |

Kutakuwa na shughuli moja ya CSL kwa mwaka. Masuala makuu ya CSL jumuishi yatatokana na kategoria pana za masuala mtambuko na ujuzi unaolengwa katika masomo mbalimbali. Walimu wanatarajiwa kuwa na masuala tofautitofauti yanayolengwa kila mwaka ili kuwapa fursa

wanafunzi walio na changamoto za kuona kutalii masuala mtambuko mbalimbali. Kunafaa kuwa na uhusiano kati ya stadi za masomo na masuala makuu.

Shughuli ya CSL jumuishi itakuwa ya shule nzima ambapo jamii yote ya shule itahusika (wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika kupanga na kutekeleza shughuli ya CSL. Ingawa walimu huongoza upangaji na utekelezaji wa shughuli ya CSL, wanafunzi walio na changamoto za kuona watatarajiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.

Shughuli hii ya CSL hutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatarajiwa kulenga umilisi na maadili tofautitofauti.

**Tathmini ya shughuli ya CSL**

Tathmini ya CSL jumuishi italenga vipengele 3 ambavyo ni: stadi kutokana na masomo mbalimbali yatakayojumuishwa katika shughuli hii, umilisi wa kimsingi uliokuzwa na maadili yaliyokuzwa. Tathmini inafaa kulenga mchakato mzima wa utekelezaji na matokeo ya mwisho ya shughuli. Mwalimu atatathmini wanafunzi walio na changamoto za kuona katika vikundi akitumia vifaa mbalimbali kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, kiwango cha ukadiriaji na vifaa vingine faafu vya tathmini.

**KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| MADA | MAPENDEKEZO YA MBINU ZA KUTATHMINI | MAPENDEKEZO YA NYENZO ZA UJIFUNZAJI | MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI |
|---|---|---|---|
| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v. ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | • Chati/kadi za breli<br>• Michoro na picha<br>• Maelezo ya michoro na picha<br>• Mgeni mwalikwa<br>• vifaa vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi(k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>• Mti maneno<br>• Kapu maneno<br>• Vitabu mbalimbali vyenye fonti zifaazo<br>• Vitabu vya breli | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **KUSOMA** | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa<br>b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kusoma kwa sauti<br>e) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>f) Potfolio<br>g) Shajara | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti chenye teknolojia saidizi<br>• Rununu yenye teknolojia saidizi<br>• Projekta<br>• Kamusi mbalimbali yenye fonti ifaayo | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |
| **KUANDIKA** | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potfolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya maelekezo<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi<br>• Barua pepe | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali vyenye teknolojia saidizi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **SARUFI** | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kutunga sentensi<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi vyenye teknolojia saidizi<br>• Kinasasauti chenye teknolojia saidizi<br>• Rununu yenye teknolojia saidizi<br>• projekta<br>• Kapu maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi maneno<br>• Picha za vitu mbalimbali<br>• Maelezo ya picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro/maelezo ya michoro<br>• Chati/kadi za breli<br>• Nyenzo halisi | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |